

Ee Baba mikononi mwako.

Na. Edwrd Daniel Challe
Rivesed Jan 2020

Wimbo wa katikati
Ijumaa kuu

$\text{♩} = 70$

Ee Ba ba miko no nimwa ko na i we kar o ho na i we kar o ho ya____ ngu, Ee Ba ba. ngu.
Ba ba

7

1. Nimekukimbilia wewe, Bwana Nisiaibike milele/

Kwa haki yako uniponye,

Mikononi mwako naiweka roho yangu;

Umenikomboa, Ee Bwana, Mungu wa kweli.

2. Kwa sababu ya watesi wangu nimekuwa laumu,

Naam, hasa kwa jirani zangu/

Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu;

Walioniona njiani walnikimbia.

3. Nimesahauliwa kama mfu asiyekumbukwa;

Nimekuwa kama chombo kilichovunjika/

Maana nimesikia masingizio ya wengi;

Hofu ziko pande zote.

4. Lakini mimi nakutumaini wewe, Bwana,

Niseme, wewe ndiwe Mungu wangu/

Nyakati zangu zimo mikononi mwako;

Uniponye na adui zangu, nao wanaonifuatia.

5. Umwangaze mtumishi wako kwa nuru ya uso wako;

Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako/

Iweni hodari, mpige moyo konde,

Ninyi nyote mnao mngoja Bwana.